African Union

Uma iniciativa do Departamento de Comissão de União Africano de

TAARIFA FUPI

# KATIKA KUUNGA MKONO IDHINI YA STC YA AU KUHUSU AFYA, LISHE NA UDHIBITI WA DAWA

## Uboreshaji wa virutubishi vya mazao ya chakula: Mkakati kamilishi unaoweza kukomesha "Njaa Fiche" Barani Afrika

### ITUBISHI VYA MAZAO

Ni mchakato wa kuzalisha mazao ya chakula kikawaida ambayo yanaongezewa vijirutubishi kiasili.

Uboreshaji wa virutubishi vya mazao ni kipengele kimoja cha utafiti wa kitaifa wa kilimo wenye kuzingatia zaidi lishe pamoja na mkakati wa uwekezaji.

Inazifaidi hasa familia za kilimo cha kiwango kidogo ambazo hutegemea mazao makuu kwa sehemu kubwa ya mlo wao na ambao wana uwezo mdogo wa kufikia njia muhimu za uboreshaji wa lishe.

Taarifa hii fupi inatoa ushahidi thabiti kuhusu jinsi uboreshaji wa virutubishi vya mazao unavyochangia lishe bora. Taarifa hii pia inasisitizia mzigo wa ukosefu wa vijirutubishi, na inapendekeza hatua kipaumbele kwa nchi wanachana wa African Union.

### TUA KIPAUMBELE


Idhini ya Kamati Maalum ya Kiufundi ya Mawaziri wa Afya wa African Union ya kutumia uboreshaji wa virutubishi vya mazao: Mawaziri wa Afya wanahimizwa kukubali idhini ya bara zima inayotambua uboreshaji wa virutubishi vya mazao kama suluhisho la kiasili lisilo na gharama kubwa na endelevu, linalolenga kupunguza utapiamlo unaotokana na ukosefu wa vijirutubishi barani Afrika. Idhini hii ya kiwango cha juu ingetoa ishara thabiti kwa Mataifa Wanachama wa AU na hivyo kuongeza kasi ya watu kufikia mikakati nyeti ya uingiliaji kati kwa kilimo chenye kuzingatia lishe. Nchi kumi na nne wanachama wa AU zimekwisha ingiza mpango wa uboreshaji wa virutubishi vya mazao katika sera na mipango yao rasmi. Idhini ya bara zima ingeongeza kasi ya kukubalika kwa mpango huo na mataifa mengine wanachama, na hivyo kuongeza ufikiaji wa mpango huu wa uboreshaji wa virutubishi vya mazao kwa wale ambao wangefaidika zaidi.

### "Njaa Fiche": Tatizo msingi

- Ukosefu wa kudumu wa vijirutubishi ni msingi wa njaa barani Afrika, na unatishia kuzuia juhudi za maendeleo.

"Njaa Fiche" ni kali sana miongoni mwa watu wanaoishi vijijini pamoja na watu wengine walio katika hatari katika mkoa wa Afrika chini ya jangwa la Sahara, hasa wanawake wa umri wa kuweza kuzaa na watoto wachanga

∆ 1 miongoni mwa watu 4 wana lishe chini ya kiwango
∆ 44% ya watoto wa shule za chekechea wanasumbuliwa na ukosefu wa vijirutubishi
∆ 24% ya vifo vinahusishwa na ukosefu wa vitamini A
∆ 39% ya wanawake wa umri wa kuweza kuzaa wana anemia
∆ Jumla ya milioni 163 ya watoto na wanawake wenye umri wa kuweza kuzaa wana anemia
∆ Mtoto 1 miongoni mwa watoto 3 chini ya miaka mitano amedumaa (44% wakiwa Mashariki, 36% wakiwa Magharibi mwa Afrika)
∆ Ueneaji wa hali ya kudumaa katika eneo la Afrika chini ya jangwa la Sahara ulipungua kwa 7.2% peke yake tangu 1985 hadi 2016.




### Athari za ukosefu wa vijirutubishi

Ushahidi ambao umepitiwa na wataalam wengine na kuchapishwa (mwingi ukiwa umefanywa barani Afrika) umeonyesha kwamba mazao ambayo virutubishi vyake vimeboreshwa ni suluhisho ambalo halina gharama kubwa, ni endelevu, na pia linalofaa kwa kuboresha lishe na afya.

Matokeo ya jumla kuhusu jinsi uboreshaji wa virutubishi vya mazao unavyopunguza ukosefu wa vitamin A

- Asilimia 50-100 ya mahitaji ya wastani ya vitamini A ya mtoto inaweza kupatikana kwa kula mazao makuu ya mahali ambayo virutubishi vyake vimeboreshwa kwa vitamini A kama mahindi, muhogo, na viazi vitamu.
- Kula viazi vyenye vitamin A vya manjano (vyenye rangi) kila siku kulipunguza ueneaji na muda wa kuhara miongoni mwa watoto na uwezekano wa kukosa vitamini A miongoni mwa wanawake.

Imefadhiliwa na:

HarvestPlus
Better Crops • Better Nutrition

Wakishirikiana na:

NEPAD
TRANSFORMING AFRICA

Food and Agriculture Organization of the United Nations

WFP
World Food Programme
wfp.org

FARA
Forum for Agricultural Research in Africa

CIP
INTERNATIONAL POTATO CENTER
A CGIAR RESEARCH CENTER

CGIAR
RESEARCH PROGRAM ON Agriculture for Nutrition and Health
Led by IFPRI

ASARECA
Transforming Agriculture for Improved Livelihoods

•Kula mahindi ya rangi ya manjano yenye vitamini A kwa miezi sita kuliongeza sana uwezo wa hisi ya kuona miongoni mwa watoto.

•Watoto ambao walikula muhogo wenye vitamini A uliochemshwa walionyesha maendeleo ya wastani lakini ya muhimu ya hadhi ya vitamini A. Tafiti zinazochunguza ubakizaji zimeonyesha kwamba muhogo wenye vitamini A uliochemshwa unaweza kuwapatia watoto asilimia 100 ya mahitaji yao ya kila siku ya vitamini A, ukiliwa kama chakula kikuu cha mahali.

### Matokeo ya jumla kuhusu jinsi uboreshaji wa virutubishi vya mazao unavyopunguza ukosefu wa iron

•Maharagwe yenye Iron na ulezi aina ya 'pearl millet' vinatoa mpaka asilimia 80% ya mahitaji ya kawaida ya watoto wachanga ya iron pamoja na wanawake wasionyonyesha, wasio na mimba.

•Yalipowa kila siku, maharagwe yenye iron— ambayo huwa na kiasi cha iron zaidi ya mara mbili kuliko aina za kawaida—yalisaidia kuzuia na kugeuza ukosefu wa iron miongoni mwa vijana wanawake. Pia yalisaidia kuboresha kumbukumbu, umakini, na uwezo mwingine wa utambuzi ambao ni wa muhimu sana katika kufikia uwezo kamili shuleni, kazi, na maisha.

•Ulezi aina ya Iron pearl millet, ambao karibuni uliletwa Afrika ulisuluhisha tatizo la ukosefu wa iron miongoni mwa watoto wa shule na pia ukaboresha uwezo wao wa kukumbuka na umakini.

### Matokeo ya jumla kuhusu jinsi uboreshaji wa virutubishi vya mazao unavyopunguza ukosefu wa zinki

•Ngano ambayo virutubishi vyake vimeboreshwa kwa zinki pamoja na mchele wenye zinki vinaweza kutoa hadi asilimia 50 ya mahitaji ya kawaida ya zinki ya watoto na wanawake wenye umri wa kuweza kuzaa.

•Watoto wachanga ambao walikula chakula kilichopikwa kwa ngano yenye zinki waliweza kuendelea na maisha yao bila kuugua kwa nimonia na kutapika kuliko watoto waliokula ngano ya kawaida.

•Kula 4 mg za zinki zaidi kila siku – kiasi ambacho uboreshaji wa virutubishi vya mazao unaweza kutoa kwa jamii zinazokula wali na ngano kama vyakula kikuu vya mahali – kunaweza kupunguza hali ya uchakavu wa DNA.

### Suluhisho kwa tishio la "Njaa fiche" kwa msingi wa ushahidi na lenye gharama ndogo

•Kwa kutumia mbinu za kawaida za uzalishaji mazao, zaidi ya aina 290 za mazao ya chakula yenye virutubishi vingi imefanyiwa majaribio na kutolewa katika nchi 60 duniani kote.

Zaidi ya watu milioni 50 katika kaya za vijijini sasa wanakula vyakula hivi ambavyo vinaleta afya bora zaidi.

Data iliyozalishwa nchini Uganda inaonyesha kwamba uboreshaji wa virutubishi vya mazao unagharimu dola $15–$20 kwa kila mwaka ambao ungepotezwa kwa ajili ya ugonjwa, ikimaanisha kwamba hii ni hatua inayofaa ya uingiliaji kati kwenye kilimo chenye kuzingatia lishe na yenye gharama inayofaa.

## MPANGO WA **MPANGO WA UBORESHAJI WA VIRUTUBISHI VYA MAZAO: KUCHANGIA KWA UTIMIZAJI WA SERA/NDOTO YA AU IFUATAYO**

Mpango wa uboreshaji wa virutubishi vya mazao unachangia kwenye utimizaji wa Ajenda 2063 ("Afrika tunayoitaka"):

∆ Kinachotamaniwa 1 (Afrika iliyositawi kwa msingi wa ukuaji na maendeleo endelevu yanayoshirikisha wote): "Visa vya njaa na utapiamlo viwe vimepunguzwa kwa angalau 80% na njaa kwa angalau 30% hasa kwa kusisitiza wanawake"

∆ Pa kuweka kipaumbele: (Afya na Lishe): Lengo 3"Raia wenye afya na lishe bora"
∆ Tokeo muhimu sana la kimageuzi: "Vifo vya mama wazazi, watoto wakiwa wachanga na watoto ambao ndio wamezaliwa vinavyotokana na utapiamlo, kama ilivyokuwa mwaka 2013 vingepunguzwa kwa nusu ifikapo mwaka 2023"

- Ahadi ya Malabo # 3 (Kukomesha njaa ifikapo mwaka wa 2025):
∆ "Komesha njaa, punguza hali ya kudumaa mpaka chini ya 10% ifikapo 2025"

- Mpango wa AU wa DREA wa Biashara na Utekelezaji wa 2017-2021:
∆ Mpango mdogo 3.4: "mpango uliopanuliwa wa uboreshaji wa virutubishi vya mazao na mifumo ya chakula".

## MAMBO AMBAYO MAMBO AMBAYO AU IMEFANYA KUHUSU UBORESHAJI WA VIRUTUBISHI VYA MAZAO KUFIKIA SASA:

- **Mkutano wa pili wa AU wa Kamati ya Kiufundi Kuhusu Kilimo, Maendeleo ya Vijijini, Maji na Mazingira mwezi wa Oktoba 2017 uliidhinisha** uboreshaji wa virutubishi vya mazao chini ya **STC/ARDWE/MIN49.** Kamati ilitaja kwamba "uboreshaji virutubishi vya mazao unakamilisha uboreshaji wa kiviwanda, kuongeza vijalizo kwenye mlo, na uanuwai wa mlo. Pia uboreshaji wa virutubishi vya mazao una uwezo mkubwa wa kuchangia sana kwenye lengo la Azimio la Malabo la AU linalokusudia kupunguza hali ya kudumaa mpaka asilimia 10 na wale chini ya uzito mpaka asilimia 5 ifikapo 2025".
- **Baraza Tendaji la AU, katika Kikao chake cha Thelathini na mbili (Januari 22-26, 2018, Addis Ababa, Ethiopia) Kumbukumbu EX.CL/1041 (XXX11),** liliidhinisha pendekezo la STC lililotajwa awali kuhusu Kilimo, Maendeleo Vijijini, Maji na Mazingira.
- **Mkutano wa Kikosi cha 10 cha Africa kuhusu Chakula na uendelezaji wa Chakula na Lishe (Juni 19-21, 2018, Bujumbura, Burundi) ulipendekeza kwa:** kuidhinishwa kwa uboreshaji wa virutubishi vya mazao ukifanywa na Kamati Maalum ya Kiufundi kuhusu Afya, Lishe na Udhibiti wa dawa ambao ungefanywa mwaka wa 2019. HarvestPlus ilipendekezwa kufanya kazi na serikali ya Burundi, nchi mwanachama wa AU na mwenyeji wa ATFFND, AUC DSA ya 10, na wabia wake kuelekea idhini ya STC ya Mawaziri wa Afya kuhusu uboreshaji wa virutubishi vya mazao.

## MUHTASARI WA MAPENDEKEZO KWA WANAOTUNGA SERA

1- Hakikisha uongozi, ahadi na upangaji kimkakati: Ili kupata maendeleo katika uanja huu, ni muhimu sana serikali ziweke katika nafasi ya juu upatikanaji wa mazao ambayo virutubishi vyake vimeboreshewa pamoja na vyakula vingine vyenye virutubishi vingi katika ajenda ya kisiasa, kuunga mkono upangaji kimkakati, sera dhahiri na kuhakikisha upatikanaji wa fedha kwenye Bajeti ya Taifa. Ili kuzidisha kabisa manufaa ya kijamii-kiuchumi, ni muhimu kutambua nyanja ambazo zinatakiwa kuwekwa kipaumbele, kama vile usambazaji wa mazao ambayo virutubishi vyake vimeboreshwa katika vituo vya afya, shule na sekta zalishaji na vilevile elimu ya lishe.

2- Wezesha utungaji na uendelezaji wa mwongozo wa kitaifa kuhusu uboreshaji wa virutubishi vya mazao, usajili, uthibitishaji na uzalishaji wa mbegu au vipandikizi ambavyo virutubishi vyake vimeboreshwa ili sekta za kibinafsi na za umma ziweze kuzidisha kiasi pamoja na usambazaji.

**Mazao makuu ya mahali ambayo virutubishi vyake vimeboreshwa yana vitu vingine zaidi ya kalori tu. Uboreshaji wa virutubishi vya mazao unatoa suluhisho endelevu kuongeza upatikanaji wa vitamini na madini kwa watu ambao hutegemea mazao makuu ya mahali kwa kiasi kikubwa cha mlo wao.**

African Union Commission | Department of Rural Economy and Agriculture
S.L.P Box 3243 Roosevelt Street (Old Ariport), W21K19
Addis Ababa - Ethiopia Simu: (251) 115 517700 Faksi: (251) 115 517874.

HarvestPlus I Melhores Colheitas • Better Nutrition C/o
IFPRI 1201 Eye St, NW, Washington, DC, 20005, EUA
HarvestPlus@cgiar.org | www.HarvestPlus.org